# JUMUIYA YA MAAFISA TAWALA NA RASILIMALIWATU TANZANIA (TAPAHR)

# KANUNI ZA UENDESHAJI WA JUMUIYA YA MAAFISA TAWALA NA RASILIMALIWATU TANZANIA,

2023

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

Contents


1.0 Utangulizi ........................................................................ 1
2.0 Uendeshaji wa Jumuiya ........................................................ 1
3.0 Haki na wajibu wa wanajumuiya/wanachama ............................... 1
4.0 Kamati za Uongozi ................................................................ 2
5.0 Uchaguzi mkuu wa Jumuiya .................................................... 3
6.0 Kugombea uongozi katika Jumuiya na sifa zake................................ 3
7.0 Viongozi/wajumbe wanaomaliza muda wao ..................................... 4
8.0 Kamati ya Uchaguzi na Usimamizi................................................. 4
(b)USIMAMIZI WA UCHAGUZI.......................................................... 4
9.0 Marekebisho ya Kanuni............................................................... 5
10.0 Kuidhinisha na muda wa kuanza kutumika ................................. 5



REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## 1.0 Utangulizi

Kanuni hizi zimetungwa kwa kuzingatia matakwa ya Wanajumuiya wenyewe kwa ajili ya Maendeleo yao na Umoja wao. Kanuni hizi zitasomwa sambamba na Katiba ya Jumuiya.

Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za uendeshaji wa Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu (TAPAHR). Kanuni hizi zimeandaliwa kwa mujibu wa Ibara ya 25 ya Katiba ya Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu inayotamka kuwa;

> Kutakuwa na Kanuni za uendeshaji Jumuiya ambazo zitaainisha uendeshaji wa Jumuiya pamoja na majukumu ya kila siku ya viongozi, utunzaji fedha, uwekaji na utunzaji wa kumbukumbu pamoja na uendeshaji wa shughuli za Jumuiya pamoja na miradi.

Aidha, Kanuni hizi zitasomwa sambamba na Katiba ya Jumuiya na endapo kukatokea mgongano kati ya Katiba na Kanuni, Katiba ya Jumuiya ndiyo itakayosimama.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## 2.0 Uendeshaji wa Jumuiya

Jumuiya ya Maafisa Tawala na Rasilimaliwatu Tanzania itaendeshwa kwa kufuata Katiba iliyopo kwa kuzingatia misingi ya usawa na haki kwa wanachama wake. Uendeshaji wa Jumuiya utazingatia misingi ya uongozi utakaowekwa na wanachama, kamati ya utendaji, Sekretarieti na kamati mbalimbali zitakazoundwa kulingana na mahitaji ya wakati na mabadiliko.

## 3.0 Haki na wajibu wa wanajumuiya/wanachama

i. Haki ya kupata fursa ya kubadilishana uzoefu katika masuala ya usimamizi wa Rasilimaliwatu na utawala katika Utumishi wa Umma.

ii. Kukuza ujuzi na weledi katika eneo la Utawala wa Umma miongoni mwa wanachama na wasimamizi wengine.

iii. Kuhifadhi na kusambaza taarifa za kitaaluma katika Kada ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala kwa njia ya tafiti, machapisho, mikutano,

ziara za mafunzo, makongamano ya kitaalamu, midahalo na kuweza kujiunga na mitandao ya kitaaluma (professional networks) kitaifa na kimataifa,

iv. Kusimamia maadili ya kitaaluma kwenye masuala yanayohusu Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala

v. Kulinda na kuheshimu Katiba ya Jumuiya hii

vi. Kupata fursa ya kushiriki fursa za kitaifa na kimataifa kupitia mashirika na taasisi zinazojishughulisha na ukuaji wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala

vii. Kuimarisha utekelezaji wa mifumo yenye matokeo tarajiwa na shirikishi ya kiutawala ili kufanikisha huduma bora kwa Umma.

**4.0 Kamati za Uongozi**

Kutakuwa na kamati mbalimbali zitakazosaidia uongozi katika utekelezaji wa shughuli zake ikiwemo;

**4.1 Kamati ya Fedha, Mipango na Maendeleo**

Kamati ya Fedha, Mipango na Maendeleo itaundwa kwa kuzingatia Ibara ya 18.2 ya Katiba ya Jumuiya kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza masuala yote ya fedha, miradi mbalimbali itakayoanzishwa na Jumuiya. Pamoja na Majukumu yaliyoainishwa kwenye Katiba ya Jumuiya Kamati hii itakuwa na majukumu ya msingi yafuatayo;

i) Kubuni miradi, programu na vitega uchumi mbalimbali vya Jumuiya

ii) Kupanga na kusimamia miradi kwa ufanisi

iii) Kushauri kamati tendaji juu ya uanzishaji na uendelezaji wa miradi

iv) Kuandaa program za Jumuiya kwa mwaka na kuziwasilisha kwa kamati tendajiKuandaa na kuratibu shughuli za kijamii zitakazofanywa na Jumuiya kwa mwaka

v) Kupanga, kuratibu na kusimamia safari za Jumuiya



REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P.O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

vi) Kutoa taarifa kwa maandishi kwa kamati ya utendaji juu ya mipango na maendeleo ya Jumuiya mara kwa mara

### 4.2 Kamati ya Nidhamu na Maadili

Kamati hii itaundwa na kamati ya utendaji kwa lengo la kukuza na kusimamia nidhamu na maadili ya wanajumuiya. Ukuzaji na usimamiaji wa nidhamu utahusu;

i) kusimamia na kukuza nidhamu kwa wanajumuiya kwa ujumla
ii) uainisha makosa ya kinidhamu kwa wanajumuiya
iii) kuandaa kanuni za adhabu kwa makosa ya kinidhamu dhidi ya wanajumuiya
iv) kuitisha vikao vya nidhamu mara tu kosa la kinidhamu litakapotokea
v) kushauri au kupendekeza kwa kamati ya utendaji juu ya adhabu itakayotolewa kwa mwanajumuiya kwa makosa ya kinidhamu
vi) kusimamia muonekano na mwenendo mzuri wa Jumuiya mbele ya jamii
vii) Kutoa taarifa mara kwa mara kwa maandishi kwa kamati ya utendaji juu ya hali ya nidhamu na uadilifu ya Jumuiya

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## 5.0 Uchaguzi mkuu wa Jumuiya

Itakapofika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Viongozi, Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wataidhinisha ratiba ya Uchaguzi. Mara baada ya ratiba hiyo kuidhinishwa, Kamati ya Utendaji ya Jumuiya itaanza maandalizi ya Utekelezaji wa ratiba ya Uchaguzi chini ya Usimamizi wa Katibu Mkuu.

## 6.0 Kugombea uongozi katika Jumuiya na sifa zake

i. Viongozi wa Jumuiya watapatikana kwa taratibu za uchaguzi. Taratibuhizi zitaongozwa na Katiba, Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Jumuiya. Nafasi zote za kuchaguliwa zitatangazwa wazi, na waombaji wa nafasi hizo wataomba katika ngazi zinazohusika kwa kujaza fomu maalumu.

ii. Nafasi za uongozi wa Jumuiya zitagombewa na Mwanchama hai wa Jumuiya mwenye sifa za kugombea uongozi.

## 7.0 Viongozi/wajumbe wanaomaliza muda wao

Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Viongozi, Viongozi wote wanaomaliza muda wao kabla ya Uchaguzi kuanza watajiuzulu nyadhifa zao kupisha uchaguzi kufanyika.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS

## 8.0 Kamati ya Uchaguzi na Usimamizi

### (a) MAANDALIZI

i. Kutaundwa Kamati ya Uchaguzi katika ngazi husikaitakayopitia na kuhakiki sifa za wagombea na usahihi waujazaji wa fomu za wagombea zilizojeshwa.

ii. Wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi watateutiliwa naKamati ya Utendaji.

iii. Kamati itakuwa na wajumbe watano, watakaojichagulia Mwenyekiti

iv. Kamati hii itatoa mrejesho kwa mgombea ambaye fomu yake ina dosari isiyokidhi masharti ya uchaguzi kupitia Mwenyekiti kda kipindi kisichozidi siku kumi na nne tangu tarehe ya mwishoya kurejeshewa kwa fomu.

v. Wagombea wa Uongozi katika ngazi zote hawatakuwa na sifa ya kuwa wajumbe wa Kamati za Maandalizi za Uchaguzi.

### (b) USIMAMIZI WA UCHAGUZI

i) Wakati wa Uchaguzi wa Viongozi, kutaundwa Kamati za Usimamizi za Uchaguzi kwa ngazi husika.

ii) Kamati ya Usimamizi itakuwa na Mwenyekiti wa muda na

wajumbe wengine wawili.

iii) Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi atakuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi.

**9.0 Marekebisho ya Kanuni**

a) Endapo kutatokea uhitaji wa marekebisho ya Kanuni hizi, wanachama watatoa mapendekezo ya maandishi ambayo yatabainisha kipengele ambacho kinakusudiwa kufanyiwa marekebisho. Mapendekezo hayo yatawasilishwa kwenye Kamati Tendaji.

b) Kamati Tendaji itajadili mapendekezo hayo na kuyawasilisha katika Mkutano Mkuu wa Jumuiya ambapo utatolewa uamuzi wa mwisho.

**10.0 Kuidhinisha na muda wa kuanza kutumika**

Kanuni hizi zimeidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Jumuiya uliofanyika tarehe 23/02/2023

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti | Katibu |
| Saini [signature] | Saini [signature] |
| Jina LEILA MAVIKA | Jina DEBORA NGANGA |
| Tarehe 23/02/2023 | Tarehe 23/02/2023 |

Kanuni hizi zimeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 23/02/2023 baada ya kupitishwa na Msajili wa vyama vya kijamii.

REGISTRAR OF SOCIETIES
21 JUN 2023
P. O. BOX 2916
DODOMA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS